

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية الجاليات بالزلفي

مشروع تعلم الإسلام – أحكام الطهارة - سواحيلي

Samo la 5

الدرس الخامس

KUPANGUSA KHOFU MBILI.

Kutokana na uzuri na wepesi wa dini ya kiislamu ni kuruhusu au kujuzisha kupangusa juu ya khofu mbili, nayo imethibiti kwa bwana mtume (saw) kwa hadithi aliyopokea Swahaba Amru bin Umayya (R.A) anasema:

فَعِنْ عُمَرَ بْنِ أُمَّةٍ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ - قَالَ: (رَأَيْتُ النَّبِيَّ - صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - يَمْسُحُ عَلَى عَمَّا مَتَهُ وَخُفْيَهُ) [رواه البخاري: 205] (Nilimuona Mtume (saw) akipangusa juu ya kilemba chake na juu ya khofu zake mbili) (Ameipokea Imam Bukhar : 205).

وعن المغيرة بن شعبة - رضي الله عنه . قال: (بینا أنا مع رسول الله - صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَسَلَّمَ . ذات ليلة ، إذ نزل فقضى حاجته ، ثم جاء فصيّبت عليه من إداوة كانت معي فتوضاً ومسح على خفيه) [مشق عليه: 203، 274]

Ameipokea Swahaba Mughira bin Shu'ubah (R.A) anasema :(Wakati tukiwa mimi pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu siku moja, muda kidogo akaenda kukidhi haja yake, kisha akaja nikammiminia maji yakiyoko kwenye chombo nilichokuwa nacho akatawadha na akapangusa juu ya khofu zake) (Ameipokea Bukhar na Muslim:203, 274).

Ni sharti kwa mwenye kupangusa juu khofu zake azivae akiwa ametawadha tayari, na iwe kupangusa ni kuitisha mikono iliyolowa maji apanguse juu yake, wala asipanguse chini ya khofu.

Muda wa kupangusa kwa mkazi wa mji ni siku moja mchana na usiku yaani masaa 24 tu, na muda wa kupangusa kwa msafiri ni siku tatu na masiku yake, lakini ni yule msafiri ambae safari yake ni ile ambayo anafaa kunguza swala.

Na inabatilika kupangusa juu ya khofu kwa kuisha muda wake au mtu akazivua baada ya kupangusa, au baada ya kupatwa na janaba hapo itamlazimu kuzivua ili aweze kuoga.

VYENYE KUTENGUA UDHU.

1. Chenye kutoka moja ya njia mbili (njia ya mbele au nyuma) mkojo, haja kubwa, kujamba, manii, madhiyi, wadiyi, damu nyingi,
2. kulala,
3. kula nyama ya ngamia,
4. kuzimia na kupotewa na akili.